# VVU

## na Sheria ya Jinai nchini Kanada

Unachohitaji kujua

# VVU na Sheria ya Jinai nchini Kanada

Kanusho: Maandishi yafuatayo yana maelezo ya jumla tu ya kisheria, sio ushauri wa kisheria. Ingawaje kila juhudi zimefanyika ili kuhakikisha usahihi wa tafsiri hii, hatuwezi kutoa uhakikisho kwamba hakuna mapungufu yoyote kwenye kila kipengele. Ikiwa unahitaji taarifa maalum kuhusu hali yako mwenyewe, tafadhali zungumza na mwanasheria.

Mara nyingi, iwapo unawaambia wengine (au "kufichua") kuwa una VVU, hiyo ni hiari yako. Unaweza kuchagua kutofichua kwamba una VVU kwa sababu huna uhakika wa jinsi ya kuwaambia watu, au kwa sababu ya unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na VVU. Unaweza pia kuchagua kutofichua kwa sababu ya ubaguzi wa rangi dhidi ya Watu Weusi, chuki dhidi ya watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja, chuki dhidi ya watu walio na utambulishaji tofauoti na jinsia ya kuzaliwa, au ubaguzi dhidi ya watu wenye roho ya kiume na ya kike.

Hali ni tofauti linapokuja kwenye suala la wenzi wa ngono. Nchini Kanada, sheria ya jinai inasema kwamba, katika mazingira fulani, lazima uwaambie wenzi wako wa ngono kwamba una VVU *kabla ya kujamiiana*. Hii wakati mwingine hujulikana kama "**wajibu wa kisheria kufichua**." Ingawa sheria ya jinai nchini Kanada mara nyingi hutumika na kutekelezwa kwa njia za kibaguzi ambazo zinaathiri isivyo uwiano watu wa Afrika, Karibeani na Watu Weusi (ACB), bado ni sheria inayotekelezwa kwa sasa.

Lakini hulazimiki wakati wote kufichua kwa mwenzi wako wa kingono kwamba una VVU chini ya sheria ya jinai. Kwa mujibu wa mahakama nchini Kanada, unatakiwa tu kumwambia mwenzi wako wa ngono kwamba una VVU kabla ya kujamiiana endapo kuna "**uwezekano wa kweli**" kwamba unaweza kumwambukiza (kusambaza) VVU. Ikiwa hutamwambia mwenzi wako wa ngono kwamba una VVU kabla ya kujamiiana ambapo kuna "uwezekano halisi" wa kuambukizwa VVU, unaweza kushtakiwa kwa unyanyasaji wa kijinsia uliokithiri, hata kama mwenzi wako hajapata VVU.

Kwa bahati mbaya, mahakama hazijafafanua kwa uwazi maana ya "uwezekano wa kweli" kwa aina mbali mbali za ngono. Kwa hivyo wakati mwingine inaweza kuwa vigumu sana kujua ikiwa una jukumu la kisheria kufichua.

# Wakati ambapo hakuna wajibu wa kufichua

- Hulazimiki kisheria kumwambia mwenzi wako kwamba una VVU kabla ya kubusiana au shughuli nyingine ambazo hazina hatari ya kuambukizwa VVU.
- Hulazimiki kisheria kumwambia mwenzi wako kabla ya kufanya ngono ya ukeni, ya haja kibwa au ya mdomo ikiwa unatumia kondomu **na** kiwango chako cha virusi kipo chini, kimekandamizwa, au hakionekani.

**Kiwango cha virusi** ni kiasi cha VVU katika majimaji ya mwili wa mtu. Kwa kawaida hupimwa kwa mililita za damu. Mojawapo ya malengo ya matibabu ya VVU ni kupunguza kiwango cha virusi kwa mtu kwa kadri iwezekanavyo, ili hatimae kuwa na virusi vichache vinavyosababisha uharibifu wa mfumo wa kinga na viungo vya mtu. Wakati mtu anapokuwa na kiwango cha virusi "kilichokandamizwa" au "kisichoonekana", hiyo haimaanishi kwamba ameponywa VVU. Lakini inamaanisha kwamba hawawezi kuambukiza VVU kwa njia ya ngono.

- **Kiwango cha chini cha virusi** inamaanisha, kwa madhumuni ya sheria ya jinai, ni kiwango cha virusi kilicho chini ya nakala 1,500 za VVU kwa mililita moja ya damu.
- **Kiwango cha virusi kilichokandamizwa** inamaanisha ni kiwango cha virusi kilicho chini ya nakala 200 za VVU kwa mililita moja ya damu.
- **Kiwango cha virusi kisichoonekana** inamaanisha kiwango cha virusi cha mtu ni kidogo sana kiasi kwamba VVU havionekani kwenye vipimo vya kutambua kiwango cha virusi.



# Hakuna uwazi iwapo utalazimika kufichua hali yako katika mazingira mengine.

- Katika miaka ya karibuni, ikitegemea na mahali unapoishi nchini Kanada, **sio lazima ufichue ikiwa una virusi vilivyokandamizwa au visivyoonekana kwa muda fulani** (kwa mfano miezi minne au sita), hata kama kondomu haijavaliwa wakati wa kufanya ngono ya haja kubwa, ngono ya ukeni, au kwa njia ya mdomo.
- Ikiwa huna kiwango cha chini cha virusi, kilichokandamizwa, au kisichoonekana **na** kondomu inatumiwa wakati wa kujamiiana kwa njia ya uke, haja kubwa, au ngono ya mdomo, na endapo una jukumu la kufichua au , kutofichua inategemea na mazingira na mahali unapoishi:
- Huko Yukon, Maeneo ya Kaskazini Magharibi, na Nunavut, sera ya shirikisho inawaambia waendesha mashtaka kwamba, "kwa ujumla" watu hawapaswi kufunguliwa mashtaka ikiwa kondomu ilivaliwa au walishiriki tu ngono ya mdomo, lakini bado watu wanaweza kufunguliwa mashtaka.
- Katika British Columbia, sera ya jimbo inasema kwamba kutumia kondomu "inaweza" kuwa sababu ya kutowafungulia watu mashtaka kwa kutowaambia wenzi wao wa ngono, lakini watu bado wanaweza kufunguliwa mashtaka. Sera pia inaeleza kwamba watu hawatafunguliwa mashtaka ikiwa tu wanafanya ngono ya mdomo na hakuna "sababu zingine hatarishi" ambazo zipo. Sera inaelezea vidonda mdomoni, ukeni au kwenye uume, fizi zinazovuja damu, kugusa kwa mdomo damu ya hedhi, na uwepo wa magonjwa mengine ya zinaa (STIs), yote hayo ni sababu hatarishi. Kunaweza kuwa na sababu zingine hatarishi ambazo waendesha mashtaka wanaweza kuzingatia, na hiyo ikiwa na maana kwamba watu bado wanaweza kufunguliwa mashtaka hata kama walichofanya ni ngono ya mdomo tu.
- Huko Nova Scotia, uamuzi mmoja wa mahakama ulisema kutumia kondomu kunamaanisha hakuna wajibu wa kisheria wa kufichua hali yako. Huu ni uamuzi muhimu. Hata hivyo, hiyo haizuii moja kwa moja kushtakiwa au kuhukumiwa katika kesi nyingine ambapo mtu alitumia kondomu lakini hakumwambia mwezi wake wa ngono kuwa ana VVU.
- Hapa Ontario, uamuzi wa mahakama wa mwaka 2020 ulisema kwamba kutumia tu kondomu sio sababu tosha ya kuwalinda watu dhidi ya kufunguliwa mashtaka na kuhukumiwa. Isipokuwa kama una kiwango cha chini cha virusi, virusi vilivyokandamizwa, au visivyoonekana, vinginevyo bado unapaswa kisheria kufichua kwa mwenzi wako wa ngono kwamba una VVU hata kama kondomu inatumiwa kufanya ngono ya ukeni na ya haja kubwa. Na hata kama umefanya ngono ya mdomo tu, isipokuwa kama kiwango chako cha virusi ni kidogo, kimekandamizwa, au hakionekani, vinginevyo bado kuna hatari ya kufunguliwa mashtaka na kuhukumiwa endapo hutamwambia mwenzi wako wa ngono - na hii inaweza kukutokea hata kama unatumia kondomu. Kutumia kondomu kwa ngono ya mdomo kunaweza kupunguza uwezekano wa kushtakiwa na kuhukumiwa, lakini hatujui kwa uhakika.

**Iwapo utatishiwa mashtaka ya jinai, tafadhali wasiliana na mwanasheria haraka sana.** Endapo polisi watataka kukuuliza maswali, sio lazima uwajibu. Unapaswa tu kuwaambia polisi jina lako na tarehe ya kuzaliwa, lakini si zaidi ya hayo, hata kama wanaendelea kuuliza maswali. Chochote utakachowaambia polisi wakati wowote kinaweza kutumika kama ushahidi dhidi yako. Una haki ya kuzungumza na mwanasheria faraghani kabla ya kujibu maswali kutoka kwa polisi. Mwanasheria ndiye mtu pekee unayepaswa kuzungumza naye kuhusu hali hii.

**Unaweza kusoma zaidi kuhusu VVU na sheria ya jinai nchini Kanada katika kijitabu chetu kirefu, kinachopatikana kwa lugha ya Kiingereza na Kifaransa.**

Mwongozo huu uliandikwa mnamo Septemba 2023.
**Tunatambua usaidizi wa kifedha wa Idara ya Haki Kanada.**

Ministère de la Justice Canada
Department of Justice Canada